Translator: Sr. Martina Marco, asc

Basi, chagua Uzima!
(Mkutano Mkuu 2011)

Habari za Kimataifa

Waabuduo Damu ya Kristo

Mwaka XIX – Namba 3, Machi 2017

Nataka kulia hata mimi...

Hapo siku za kale, wakati dunia yote ilipokuwa mpya, kipupwe kilifanya mimea yote ardhini icheze toka gizani kuelekea mwangani, na yote kuchanua mara.
Mmea mmoja tu haukusikia mwito wa kipupwe, na mwishowe wakati ulipoweza kuvunja udongo mgumu ili ucheze, kipupwe tayari kilikuwa kimeenda mbali...

"Nifanye hata mimi nichanue, ee Bwana!" – mmea uliomba. " "Wewe pia utachanua" – alijibu Bwana. "Lini?" – uliuliza kwa wasiwasi mmea mdogo usio na jina. "Siku moja..." – na jicho la Mungu lilijifumba kwa huzuni.

Mhariri

Ukawa muda mwingi umepita, kipupwe, hata mwaka ule kilikuwa kimekuja na kwa mguso wake, mimea ya Golgota ilifungua maua yao. Mimea yote, isipokuwa mmea mdogo usio na jina.

Upepo ulirudisha mwangwi wa kilio kikubwa, cha huzuni cha mimea: mwanamme mmoja alijitokeza kati ya umati wa watu, aliyepinda chini ya msalaba, alikuwa na uso wa maumivu na wenye damu... . "Nataka kulia hata mimi kama wanavyolia wanadamu" – ulifikiri mmea mdogo kwa msisimko. Wakati huo, huyo mwanaume akiteseka kwa uzito wa msalaba, mche mdogo ulipita kando yake na moja ya chozi lake yule mwanaume lililochanganyikana na damu lilidondoka juu ya mche mdogo wenye masikitiko. Mara lilichanua ua zuri sana ambalo lilikuwa na zana za mateso: taji, nyundo, misumari ...ulikuwa mmea wa matunda mateso, ua la mateso.

Mmea wa matunda mateso ulichipukia kwenye uhai kwa sababu ulijiachia uguse maumuvu ya watu na ukafungua moyo kwa zawadi ya yule lilikopopita kando yake.

Mhutasari

Mhariri
Nataka kulia hata mimi…

Nafasi kwa NGO - VIVAT
Mfano wa kuwa katika mtandao

Toka Ulimwengu ASC
Hospitali ya Mama yetu wa Guadalupe
Tuzungushie miji yetu upendo
Pamoja, kwa kuwatetea wanyonge
Mkutano kwa ajili ya wanawake walio katika malezi
Mitihani ya taifa 2016

Ndani ya Shirika
Kalenda ya Uongozi Mkuu
Waliorudi nyumbani kwa Baba

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Eneo la Bara: Amerika
Region: Brazil

Siku ya sherehe katika Hospitali ya Mama yetu wa Guadalupe

Tarehe 17 Februari mwaka huu kulikuwa na sherehe iliyofana ya ufunguzi wa gorofa ya pili ya hospitali ya Guadalupe iliyokarabatiwa, (HG), ambayo ililuwa haijatumika kwa miezi kadhaa.

Gorofa hiyo mpya ina vyumba 18 na kimoja cha huduma ya upimaji wa magonjwa ya tumbo na mfumo wa upumuaji ambamo pia inaongezeka huduma ya Oncologia na Chemiotherapy, muhimu sana kwa sababu ya ongezeko la wagonjwa wa saratani na Belem. Walikuwepo waganga wengi, wafanyakazi na watu marafiki wa hospitali. Sherehe ilianza kwa baraka ya vyumba vipya, iliyotolewa na padre Francisco, padre mkapuchini; baadaye ilifuata tafrija ya pamoja.

Masista ASC wa jumuiya ya Nyumba ya Mapokezi ya Mama yetu wa Guadalupe (Sr. Marlene, Sr. Clara na Sr. Marilia) walifurahia sana uwepo wa Sr. Ivone Freitas, mkurugensi wa Hospitali kuanzia mwaka 2010 hadi 2016, ambapo alikuwa amekuja kutoka Manaus ili kushiriki tukio kwa heshima ya kikundi kipya cha uongozi wa Hospitali.

Kikundi kipya cha uongozi kimeundwa na: aliye juu ya mkuu wa Hospitali, Sr. Marlene, Bwana Sebastião Carvalho, Mkuu; Mganga Marcos Moreno, Mkurugenzi mtendaji; Mganga Ana Emilia Magno, katibu na wakili; Bwana Alexandre Moreira, Meneja.

Kama tunavyojua, hopitali ya Guadalupe, baada ya miaka mingi ya sala, na ushauri wenye maumivu na utafiti kwa upande wa Uongozi Mkuu, region na ASC wenyeji, ilikuwa kwenye kutafuta suluhisho la kuridhisha kwa changamoto ya kazi kubwa – zaidi ya yote changamoto ya kuanguka kwa uchumu hali ambayo Brazil inakumbana nayo – inayoonekana kuibua nyakati ngumu zaidi.

Sr. Marlene na Sr. Ivone waligundua jiwe lililo na jina la "Mtakatifu Maria De Mattias" ambapo liliwekwa wakfu upya kwa heshima ya Masista Waabuduo Damu ya Kristo. Sr. Ivone alikishukuru kikundi cha uongozi akithibitisha kuwa kwa ufunguzi wa gorofa nzuri ya pili, ndoto ya watu wengi imetimia kwa ajili ya utunzaji wa afya za watu wetu. Padre Francisco alikisifu kikundi, akikazia kazi ya wakristo, walei na wasio, Neno la Mwinjili Matayo (Mt. 6:13 – 16) ninyi ni "chumvi ya ulimwengu" na alithibitisha kuwa hospitali, ambayo inafurahia ulinzi wa Mama yetu wa Guadalupe, itaendeleza huduma yake kwa manufaa ya watu wetu.

Bwana Sebastião alikazia kuwa, ili kutoa huduma zinazofaa na kuendelea kufanya utume mzuri wa Hospitali ya Mama yetu wa Guadalupe ni lazima wote kuungana.

Sr Marilia Menezes, asc

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Eneo la Bara: Amerika
Region: USA

Tuzungushie miji yetu upendo

Waabuduo wa Damu ya Kristo wa Nyumba ya Wichita waliwaalika watu wengine kuungana nao kwenye sala ya kitaifa inayojulikana kama "tuzungushie miji yetu upendo", iliyofanyika kwenye kikanisa cha Nyumba yetu kuanzia saa nane hadi saa nane na nusu mchana siku ya jumapili tarehe 15 Januari.

Washiriki wakiungana na mataifa yote wametuma kupitia tafakari na ukimya, nguvu ya upendo ambao unaleta uponyaji, amani na haki kwenye miji yetu, kwenye nchi yetu na kwa dunia yetu, siku ileile ya kusimikwa Rais Trump na ya maandamano yaliyofuata.

Tukio lilikuwa ni mfululizo wa Tuzungushie miji upendo ambalo lilifanyika huko Cleveland, kiangazi kilichopita, kabla ya mkutano wa kitaifa wa watu wote.

Utaratibu uliofuata ulikuwa wa kawaida sana. Tulijiweka kwenye mduara kama mashahidi wakimya tukiungana na mataifa mengine yote, muda ule ule. Mdundo wa kawaida ulisikia wakati wa mwanzo na wa mwisho wa sala. Japo ilikuwa siku ya Baridi, na barabara zilizofunikwa na theluji, walikuja kuungana nasi watu mbalimbali: wanachama wa damu, waumini wa makanisa mengine na marafiki wa masista, kwenye muduara uliokuwa na jumla ya washiriki 36.

Sr Joann Stuever, asc
Sr. Fran Schumer, asc



ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Eneo la Bara: Amerika
Region: USA

Pamoja, kwa kuwatetea wanyonge

Waabuduo na wakereketwa wao waliungana kukataa amri ya nguvu ya rais Trump kuhusu kupiga marufuku kuingia USA kwa baadhi ya wahamiaji.

Sr. Joan Hornick, ASC na Cecilia Hellmann, ASC na wakereketwa wengine, tarehe 31 Januari, huko Belleville, Illinois, walikutana kwenye uwanja antistante ofisi ya Mike Bost., US Rep.

Walikuja pia wanachama wa damu Ada Jimenez na mwanachama mpya wa damu Teresa Jimenez Nickerson.

Sr. Cecilia Hellmann akiwa ameshikilia karatasi kubwa iliyoandikwa “kataa”.

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Eneo la Bara: Amerika
Region: USA

Pamoja, kwa kuwatetea wanyonge

Waabuduo, Walei wanachama wa Damu, wanaofanya kazi nasi na marafiki walishiriki maonyesho ya siku ya wanawake duniani ya tarehe 21 Januari ili kupinga siasa zenye chuki kwa haki za watu zilizozinduliwa na rais Trump.

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Eneo la Bara: Asia
Region: India

Mkutano wa wanawake walio katika malezi

Siku zilizosubiriwa sana za mkutano wa wanawake walio katika malezi kwenye jumuiya ya Trichur-Arampilly hatimaye ziliwadia ambazo ni tarehe 29 na 30 Oktoba 2016.
Washiriki wote walifika pamoja na walikuwa na furaha sana kushiriki katika tukio hili, lililotanguliwa na matayarisho ya kutosha. Ushiriki wao hai ulizifanya hizi siku mbili kuwa za maana.

Walezi na walelewa, pamoja na wanajumuiya, walifikia santuari ya Mungu kwa huduma ya sala. Masista waliwasindikiza vijana kwenye altare ya Bwana, wakitaka kuheshimu wito wao kupitia huduma ya sala fupi lakini ya maana sana. Alama yenyewe ya dafu la nazi na maelezo yake viliwafanya vijana wafungue macho kwa kuona uzuri wa wito wao wa thamani na kutoa asante kwa Mungu kwa zawadi ya wito. Walelewa walielewa kwa kiasi kikubwa zawadi hii ya wito wakitafakari historia nzuri ya mwanamke mmoja ambaye alitaabika kwa kufungua kifuu cha nazi na ambaye mwishowe aliweza kunywa maji matamu na ya baridi kwa utoshelefu mkubwa. Kwenye somo fupi la Injili ya Marco, wito (Mk. 8, 34-38), ilifuata usomaji wa maandishi ya Mt. Maria De Mattias , mwanzilishi wetu na kusali sala ya kumwomba yeye.

Vijana walimwonyesha Mungu hamu yao ya kukua katika uaminifu na huduma ya upendo kwa Mungu, mu-umbaji.
Sr. Mini Pallipadan na Sr. Elsy Palatty waliwapa alama ya mwanamke aliyeko kwenye malezi asc, na waliipamba kwa maua na kwa orodha ya fadhila muhimu zenye kuwaletea maisha matakatifu na kumfuata Kristo kwa mtindo imara. Sala ilihitimishwa kwa utenzi wa Bikira Maria.
P. Johnson, SDB alitupa baadhi ya tafakari zake zinazohusu wito na aliongoza mafundisho mbalimbali ambapo kwa kupitia hayo vijana waliweza kufikiria upya wito wa kwanza wa safari yao ya ufuasi. P. Lawrence Olekenkil alichangia katika kufundisha thamani ya Sakramenti; yote aliyosema yalikuwa ya manufaa na ya kufungua macho ya vizazi vipya zaidi vya leo ambavyo vinatafuta ku-

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

kimbia hali halisi kwa kufanya mazoezi ya kiroho. Mwishoni Prof. Swarna alitualika kutoa shukrani kwa kwa Baba kwa zawadi za wema wake.

Mchana ilifanyika michezo nje na mashindano; masaa ya jioni yalipendezeshwa na matukio ya kiutamaduni: walelewa waliandaa ngoma za kucheza, maonyesho na mipango mingine ya burudani.

Hija ilimalizika kwa kutembelea kanisa lililojengwa kwa sheshima ya Mt. Thomaso, Mtume huko India.

Sr Hemema
Juvvannapudi, asc

Eneo la Bara: Afrika
Region: Tanzania

Mitihani ya kitaifa 2016

Ilionekana kama utani hivi wakati tulipojaza fomu zetu za kuridhia kufanya mitihani ya kitaifa, lakini ilikuwa kweli.

Tulisoma kwa bidii, vizuri kadiri tulivyoweza kwa msaada wa waalimu, masista na wafanyakazi, ili kukamilisha mada zote za kidato chetu cha pili.

Masista walitutia moyo na wenzetu walitusaidia wakichukua majukumu ya kufanya usafi wa mazingira na wakijenga hali ya maelewano na urafiki.

Jumatatu tarehe 14 Novemba tulianza mitihani yetu. Ilifanyika mitihani ya kidato cha pili ya kitaifa kwa wote walio katika kidato cha pili. Kwa sala za watu wengi tuliifanya kwa moyo. Kabla ya kuanza tulisoma vizuri sheria na taratibu za mitihani na hii iliturahisishia, kwa sababu hatukupata matatizo yoyote wakati wa mitihani. Wasimamizi walitutia moyo kwa namna ya upole na ukunjufu. Kwa msaada wa Mungu, tulimaliza mitihani na shule ilifungwa

Wakati tulipokuwa nyumbani tulikuwa na shauku ya kujua matokeo; shule ilifunguliwa tena tarehe 3 Januari 2017. Shukrani kwa Mungu kwa kutuwezesha kuanza mwaka mpya na kujikuta wote pamoja tena, hatukujua tarehe rasmi ya matokeo.

Hatimaye, asubuhi moja ya jumatatu, mkuu wa shule alitutangazia kuwa matokeo yangetoka asubuhi hiyo. Tulifurahi tulipoona kuwa wanafunzi 81 kati ya 84 walipata daraja la kwanza na watatu walipata daraja la pili. Hakuna aliyepata daraja la chini. Haya matokeo mazuri hivi yalitushangaza sana kwa sababu baadhi ya mitihani ilikuwa migumu sana, kwa namna ya pekee ule wa biashara.

Kila mwalimu, wafanyakazi na masista walitupongeza na hata wanafunzi wengine pia. Tuna shukrani kwa msaada wa Mungu na tunasubiri kujua kama shule yetu imewekwa kwenye orodha ya shule tatu za kwanza Dodoma na kwenye nafasi ya ngapi katika ngazi ya Taifa.

Wote tunaweza kusema kuwa kile tulichopata pia ni tunda la kazi ya masista ambao wanafanya kazi kwa upendo.

Wanafunzi, shule ya sekondari
Maria De Mattiaa ya Kijiji cha Matumaini

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Mfano kwa ajili ya kuwa katika mtandao

Liechtenstein ni taifa lenye ustawi. Mara nyingi, kwa mataifa tajiri au watu tajiri zipo dhana kuwa hawaangalii watu wengine. Siyo sababu katika swala hilo, kwa kuwa hapa Lichtenstein wapo watu wengi ambao wanafanya kazi katika mashirika ya kibinafsi au yao, ambao kwa nguvu nyingi na ubunifu wanajishughulisha katika miradi ya maendeleo kwa ajili ya mataifa ya kusini.

Katika baadhi ya makundi haya, hamu ya kupendelea kazi ya pamoja na ya kuunganisha nguvu inakua ni, kama inavyosema methali moja: "Kama unataka kwenda haraka, tembea peke yako, kama unataka kwenda mbali, tembea pamoja na wengine."

Mashirika 20 yameitikia kwa moyo mwaliko wa kutafuta safari moja ya pamoja. Kati ya hayo kulikuwa pia na kikundi cha VIVAT cha Schaan. Baada ya mwaka mmoja wa utafiti wa kina, tarehe 24 Januari 2017 uliundwa "Mtandao kwa ajili ya Maendeleo ya pamoja" mradi uliwasilishwa wakati wa mazungumzo ya pamoja.

Wawakilishi wa sasa wa uongozi na wa huduma ya maendeleo wa serikali walishukuru sana kwa kuzaliwa kwa mtando huu unaoundwa na mashirika binafsi.

Katika umoja huu, ilichukuliwa pia miongozo iliyofanikishwa mwanzoni. Malengo ya mtandao ni:

- Kukuza ufahamu wa umuhimu wa mshikamano wa wote na wa uhitaji wa mshikamano wa kimataifa;
- Kusaidia hamu za watu wanaokuja toka nchi zinazoendelea kupitia mawakili wa siasa na uchumi;
- Kuchochea hali ya kuthamini na wepesi wa kujishughulisha wa jamii ya Liechtenstein;
- Kujenga jukwaa kwa ajili ya mashirika yaliyomo kwa namna ambayo yataweza kufahamiana vizuri na kuunganisha shughuli zao.
- Kuimarisha mradi wa kazi za wanachama mojamoja kupitia mabadilishano ya uzoefu na malezi endelevu.

Kwenye mwanzo wa miongozo husema: "tunatambua kuwa uondoaji wa umasikini katika mifumo yake yote na viwango vyote, pale ambapo umasikini uliokithiri, iwe ni changamoto kubwa ya wote, inayoonekana kuwa ni ya lazima kwa maendeleo thabiti.

Kikundi cha VIVAT cha Schaan ni kidogo. Kupitia mtandao, wanachama wanatumaini kuwa katika kiwango cha kushirikiana kwenye mipango inayotekelezwa na mashirika makubwa zaidi. Kuunganisha nguvu, inawezekana kufanya kitu zaidi.

huko Liechtenstein, tarehe 10 Disemba 2016 kilianzishwa pia "chama kinachojitegemea kwa ajili ya haki za binadamu." Kujitegemea inamaanisha kuwa chama hakifungamani na siasa na hakishawishiwi na serikali. Kinafanya kazi katika eneo la wakimbizi, mahali ambapo watu au kikundi wanaweza kwenda kwa ajili ya kupata msaada wanapojisikia kudhulumiwa haki zao. Kama kikundi cha VIVAT, hawakutaka kuwa mmoja wa mwanachama waanzilishi, bali kushirikiana kawaida wao kwa wao katika hali zinazoonekana.

Sr. Lisbeth Reichlin ASC

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org

Kalenda ya Uongozi Mkuu

Tarehe 4 Machi:
Sr Mariamma, Sr Barb, Sr Zita na Sr Sonia watashiriki kwenye sherehe ya miaka 183 ya kumbukumbu ya Kuanzishwa Waabuduo Damu ya Kristo huko Acuto.

Mwangalie Msulubiwa, na kwa namna ya pekee kwenye Madonda yake Matakatifu... Ho! Upendo gani.. ho! Nguvu gani kwa ajili ya kuwatangazia wote amani kamili , ambayo inatoka katika madonda pendevu ya Yesu... Upendo mwanana, upendo mwanana, upendo mkubwa kwa ajili ya Yesu na kwa ajili ya kuziokoa roho na kuzipeleka kwa Yesu. Mwanangu usichoshwe kamwe na madonda ya Yesu; jifunze katika Madonda hayo namna ya kupeleka furaha kwa wote.

Maria De Mattias, 8 Agosti 1862

Waliorudi Nyumbani kwa Baba

Region Italia
14 Februari 2017
Sr Lucia Pacifico

Region Italia
14 Februari 2017
Sr Paola Chenet

Region Manaus
16 Februari 2017
Sr Maria Dolores Praia Soares

Region Italia
17 Februari 2017
Sr Chiara Fruttini

Region Usa
20 Februari 2017
Sr Loretta Gegen

Region Italia
22 Februari 2017
Sr Margherita Proietti

ASC International Communications - General Administration | Via Maria De Mattias,10–00183, Rome
Website: www.adoratrici-asc.org E-mail: redazioneasc@adoratrici-asc.org